Swahili

# Ushahidi wa Mtume kwa maswahaba wake na ubainishaji wa Ubora wao, na Mafunzo yatokanayo na Ushahidi huo.

Prof.Ayman Alasar

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu Mtukufu, anayesema katika Qurani Tukufu: {Na wale waliotangulia, wa kwanza, katika Muhajirun na Answar, na waliowafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu Mtukufu ameridhika nao na wao wameridhika naye; na amewaandalia Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu}

Na ninashuhudia kuwa hakuna mungu mwingine anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu asiye na Mshirika wake, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni Mjumbe wake na Mtume wake. Ewe Mola wetu tunakuomba umswalie na umpe rehma na umbariki yeye pamoja na Watu wake na Maswahaba wake na kila atakayewafuata kwa wema mpaka siku ya mwisho.

Na baada ya utangulizi huu;

Hakika Mwenyezi Mungu, kama anavyomchagua kwa ajili ya Ujumbe wake, amtakaye miongoni mwa waja wake, - kwa mujibu wa alivyyowaumba – kutokana na usafi wa moyo na usafi wa akili, na maumbile bora, na tabia njema, hakika yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu, anawachagulia Mitume wake mtu anayefaa kuambatana nao, kuulinda ujumbe wao, na kusimama katika kuifikisha risala yao kwa uaminifu wa hali ya juju na ukweli wa kujitolea baada yao; ambapo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Mwenyezi Mungu huteua wajumbe miongoni mwa Malaika na miongoni mwa watu. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenyekusikia, na mwenye kuona} kwa hivyo, Maswahaba wa Mtume S.A.W, ni wabora wa Umma huu kwa nyoyo, na wenye ubobezi wa Elimu ya Dini, na wasio na makuu, na wala hakuna jambo lolote la kushangaza katika hili. Kwani wao ni watu waliochaguliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili ya kusahibiana na Mtume wake S.A.W, na kuisimamisha Dini yake, na kuifikisha kwa walimwengu wote.

Hakika kuwazungumzia maswahaba wa Mtume S.A.W ni mazungumzo ya walio teuli kwa Mtume S.A.W katika wanadamu baada ya Manabii na Mitume. Kutoka kwa Ibn Abass R.A amesema: hakika watu waliochaguliwa katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: {**Sema: Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu. Na amani iwashukie waja wake aliyowateua.Je? Mweyezi Mungu ni bora, au wale wanaowashirikisha naye**} hao ni Maswahaba wa Mtume S.A.W. Na kutoka kwa Ibnu MAsoud R.A, amesema: Hakika Mwenyezi Mungu ameangalia katika nyoyo za Waja wake akamchagua Mtume yeye Mwenyewe kisha akampa ujumbe wake kisha akaangalia katika nyoyo za waja wake baada ya moyo wa Mtume S.A.W, akazikuta nyoyo za Maswahaba wa Mtume S.A.W, kuwa ni nyoyo bora za Waja wake baada ya moyo wa Mtume S.A.W. na akawajaalia kuwa Mawaziri wa Mtume wake wakiilinda Dini yake, na kwamba kile wanachokiona waislamu kuwa ni kitu kizuri basi kitu hicho kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kizuri pia, na kile wanachokiona kuwa ni kibaya, basi kwa Mwenyezi Mungu ni kibaya pia. Musnad Ahmad.

Na hapana shaka kwamba mwenyekukizingatia kitabu cha Mwenyezi Mungu anatambua kwamba Maswahaba wa Mtume S.A.W, wana nafasi ya hali ya Juu na cheo kikubwa mno na fadhila nyingi. Kwani wao ndio ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaridhia na amewashuhudia wakiwa na Imani ya kweli, ambapo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {**Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewapa radhi waumini walipofungamana naye chini ya Mti na aliyajua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao na akawalipa kwa ushindi wa karibu**}

Watu wa Tafsiri wanasema: {**na alijua yaliyomo nyoyoni mwao**} ina maana ya uvumilivu na Ukweli, na Uaminifu, Usikivu na Utiifu na uzuri wa kuona kwa mioyo yao haki ambayo Mwenyezi Mungu amewaongoa kuielekea.

Na hakika ya Mwenyezi Mungu, amewatakasa Maswahaba wa Mtume S.A.W, katika sehemu nyingi ndani ya Kitabu chake Kitakatifu, na miongoni mwa sehemu hizo ni katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: {**Waliomwitika Mwenyezi Mungu na Mtume baada ya kwishapatwa na majeraha – kwa waliofanya wema miongoni mwao na wakamcha Mwenyezi Mungu utakuwa ujira mkubwa –**

**walioambiwa na watu: kuna watu wamekukusanyikieni waogopeni! Hayo yakawazidishia imani wakasema: Mwenyezi Mungu anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa. Hakika wale walionunua ukafiri kwa imani hawatamdhuru kitu Mwenyezi Mungu, na yao wao ni adhabu chungu**}

Na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: {**Wapewe Mafakiri Muhajiriina waliotolewa majumbani mwao na mali yao kwa ajili ya kutafuta fadhila za Mwenyezi Mungu na radhi zake, na wanamsaidia Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao ndio wa kweli. Na walio na maskani zao na imani yao kabla yao wanawapenda waliohamia kwao, wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa walivyopewa Muhajiriina, bali wanawapendelea kuliko nafsi zao ingawa wao wenyewe ni wahitaji. Na mwenyekuepushwa na uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio wenyekufanikiwa**} ikiwahusu Muhajiriina na Answar, Maswahaba waliohamia Madina na Mtume S.A.W pamoja na Maswahaba wa Madina waliowanusuru wenzao.

Na kama zilivyokuja Aya nyingi za Qurani Tukufu kwa ajili ya kudumisha utajo wa Maswahaba wa Mtume S.A.W, kwa sifa za hali ya juu, na zenye uzuri wa aina yake, na heshima ya hali ya juu na iliyo bora, zimekuja Hadithi Sahihi za Mtume S.A.W pia kwa ajili ya kushuhudia nafasi ya Maswahaba kwa Mtume S.A.W, zikiweka wazi jinsi walivyojitolea, na zikaonesha malengo yao ya kweli, kwani wao ndio waliomliwaza Mtume S.A.W na wakamnusuru na kuifuata nuru ambayo alikuja nayo Mtume S.A.W, na wakayatanguliza mapenzi yao kwa Mtume S.A.W kuliko kujinda wao wenyewe, na watu wao, pamoja na watu wote, na Mtume S.A.W akawapa nishani za juu, na kuwavika mataji ya vyeo vikubwa; ambapo Mtume aliwatolea Ushahidi katika hali nyingi zilizojitokeza, akasema Mtume S.A.W: Watu walio bora zaidi ni wale wa Karne yangu, kisha wale wanaowafuatia, kisha ya wale wanaowafuatia. Hadithi hii ina cheo cha Mutafaqu Alaihi. Na anasema Mtume S.A.W: Nyota ni amana za Mbingu, zinapotoweka nyota Mbingu hujiwa na kile kilichopewa kiaga, na mimi ni amana kwa Maswahaba wangu, nitakapoondoka basi Maswahaba wangu hujiwa na kile kilichowekewa kiaga, na Maswahaba wangu ni amana kwa umma wangu, na watakapoondoka basi umma wangu utajiwa na kile kilichowekewa kiaga. Na anasema Mtume S.A.W: Mtaendelea kuwa katika heri ikiwa miongoni

mwenu yupo aliyeniona na kuambana na mimi, na akaambatana na aliyekuwa na mimi, Ninaapa mtaendelea kuwa katika heri kwa kuwa miongoni mwenu yupo aliyeambatana na aliyeniona mimi na akaambatana na aliyeambatana na mimi. Ninaapa kuwa bado mtaendelea kuwa katika heri kwa kuwa miongoni mwenu kuna aliyemwona aliyemwona aliyeniona mimi, na akaambatana na aliyeambatana na aliyeambatana na mimi. Hadithi hii imo ndani ya Kitabu cha Muswannafu Ibni Abii Shaibah. Na hawakuonwa kuwa ni wabora baada ya waliotajwa katika Hadithi hii isipokuwa kwa utukufu wa kuambatana kwao na Maswahaba wa Mtume S.A.W.

Mtume S.A.W aliwapa baadhi ya Maswahaba sifa maalumu kwa ajili ya kubainisha kutangulia kwao na kuwa kwao mbele katika fadhila, na hasa wale waliotangulia ambao ni wa mwanzo miongoni mwa Maswahaba. Anasema Mtume S.A.W: Swahaba aliye mpole mno katika Umma wangu ni Abuu Bakar, na Swahaba aliye na nguvu zaidi katika jambo la Mwenyezi Mungu katika Umma wangu ni Omar, na Swahaba mwenye aibu nyingi kuliko wote ni Othman, na Swahaba mweye uweoz mkubwa wa kutoa maamuzi ni Ali bin Abuu Twaalib, na Swahaba Mwaminifu zaidi katika Umma wangu ni Abu Ubaidah bin Jaraah, na Swahaba mwenye ujuzi zaidi wa Halali na Haramu katika Umma wangu ni Muadh bij Jabal, na Swahaba mwenye kujua kusoma zaidi ya wote ni Ubayyu, na Swahaba mwenye kuyajua mengi zaidi ya Mirathi ni Zaid. Na siku aliyopanda Mtume S.A.W  Jabali la Uhudi akiwa na Abuu Bakar, Omar na Othman R.A, Jabali likawatetemekea kwa furaha ya kuwa na Mtume S.A.W na Maswahaba wake, na Mtume akaliambia Jabal: Tulizana ewe Mlima wa Uhudi, kwani juu yako una Mtume wa Mwenyezi Mungu, na Msema kweli, na Mashahidi wawili (Mashujaa wanaofia vitani). Hadithi hii ipo katika Swahiihul Bukhariy.  Na Mtume S.A,W. amesema wakati akiweka wazi nafasi ya Abu Bakari Swidiiq na Omar R.A: Hakika watu wa vyeo vya juu wanawaona hawa kwa chini yao, kama vile inavyoonekana nyota ichomozayo katika upeo miongoni mwa peo za mbingu  na hakika Abu Bakar na Omar ni miongoni mwao na ndio walio na neema zaidi.Katika kitabu cha Sunanu Bnu Maajah.

Mtume S.A.W alikuwa na shime kubwa ya kudhihirisha nafasi na cheo cha Maswahaba wake R.Ana kuuweka wazi utukufu wao na uzito wao; kwa ajili ya kuwatia moyona kuibua ari zao, mpaka wawe ruwaza kwa

wengine miongoni mwa vizazi vya Umma huu. Anasema Mtume S.A.W: kuhusu Abu Bakar R.A: Msiniudhi kupitia Rafiki yangu kwani hakika ya Mwenyezi Mungu Mtukufu amenituma mimi kwa uongofu na Dini ya kweli, na nyinyi mkaniambia: Nimesema Uongo, na Abu Bakar akaniambia: Nimesema kweli, na kama sio Mwenyezi Mungu Mtukufu kumwita Rafiki wa kusuhubiana naye basi mimi ningelimfanya kuwa kipenzi change, lakini huu ni undugu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Imo kwa Bukharin a wengine, kwa tamko la Twabraaniy.

Na anasema Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, S.A.W: kuhusu Omar R.A: Hakika ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ameujaalia ukweli kupitia ulimi wa Omar R.A, na moyo wake. Katika Musnad Ahmad. Na anasema Mtume S.A.W kuhusu Othman R.A: hivi mimi simuonei haya mtu ambaye Malaika wanamuonea haya. Swahiihu Muslim.

Na anasema Mtume S.A.W: kuhusu Ali R.A: Wewe ni kutokana na mimi na mimi ni kutokana na wewe. Mutafaqun alaihi.

Hakika mfuatiliaji wa Hadithi za Mtume S.A.W na Maswahaba wake na jinsi anavyowatolea ushahidi, atatambua kwamba Mtume S.A.W amewatolea mifano bora kuliko yote, kwa uaminifu, upendo wa kweli, na mtangamano ulio bora zaidi kwa kwao kwa sura ambayo historia haijawahi kuwa na mfano huo. Mtume S.A.W alikuwa akiyahisi machungu yao na alikuwa akiwaonea huruma, alikuwa akimtembelea anayetoweka miongoni mwao, na anamtembelea anayeumwa, na anakuwapo katika mazishi yao, na anaukubali mwaliko wao, na anashauriana nao katika jambo lolote muhimu, na anawafungulia moyo wake kwa kuwahurumia, na anawalipia madeni yao, na anawaombea dua wao na watoto wao. Na kutoka Kwa Bi Aisha Mama wa Waumini, R.A, anasema: Mtume S.A.W aliingia nyumbani wa Othman aliyechomwa mkuki, R.A, akiwa amekufa, akamjongelea na kumbusu kisha akalia mpaka nikayaona machozi yake yakibubujika katika mashavu yake. Ipo katika Muswannaf Abdul Razaaq.

Na Mtume S.A.W aliwatembelea Maswahaba wake siku moja baada ya kumalizika moja ya vita vilivyokuwa baina yao na Washirikina, akawaambia: Je mmepotelewa na yoyote?wakasema: Ndio. Fulani na Fulani na Fulani. Kisha akasema tena: Je mmepotelewa na yoyote? Wakasema: Ndio. Tumepotelewa na Fulani na Fulani na Fulani, kisha

akasema: Je mmepotelewa na yoyote? Wakasmea: hapana. Lakini mimi nimepotelewa na Julaibiba, hebu mtafuteni, wakaenda kumtafuta katika waliofariki, na wakamkuta pembezoni mwa watu saba aliyowaua. Kisha wakamuua. Akasema Mtume S.A.W: huyu ni kutokana na mimi na mimi ni kutokana naye, huyu ni kutokana na mimi na mimi ni kutokana na huyu. Kisha Mtume S.A.W akamweka mapajani mwake, na akasema, hana huyu isipokuwa mapaja ya Mtume S.A.W, mpaka alipozikwa aliendela kuwa mapajani mwa Mtume. Hadithi hii imo katika Swahiihu Muslim.

Na anasema Mtume S.A.W: Mimi nina haki zaidi kuliko Muumini yoyote. Atakayeacha mali basi ni kwa ajili ya watu wake. Na mwenye kuacha deni au kupoteza basi ni kwangu mimi na ni juu yangu mimi. Hadithi hii imo katika Swahiihu Muslim.

Ninaisema kauli yangu hii na ninamwomba Mwenyezi Mungu msamaha kwangu na kwenu.

**

Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mlezi wa viumbe vyote. Na ninashuhudia kwamba hakuna yoyote anayestahili kuabudiwa kwa Haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, yeye pekee asiye na mshirika wake, na ninashuhudia kwamba Bwana wetu Muhammad ni Mua na ni Mtume wake, na rehma na amani ziwe juu ya Mtume wa Mwisho katika Mitume, na Manabii wake Mwenyezi Mungu Mtukufu, Bwana wetu Muhammad S.A.W, na Jamaa zake, na Maswahaba wake wote, na atakayewafuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.

Ndugu zangu Waislamu.

Mtume S.A.W ameuusia Umma wake wote juu ya Maswahaba wake wote, na akatoa onyo kali kwa wenye kuwafanyia mabaya.

Ndugu zangu Waislamu,
Mtume S.A.W ameuusia Umma wake wote juu ya Maswahaba wake na au kuwavunjia haki zao na akaweka wazi kwamba kuwapenda Maswahaba ni dalili ya kumpenda yeye mwenyewe S.A.W, na kwamba kuwachukia Maswahaba ni dalili ya kumchukia Mtume S.A.W pale aliposema: Ninakusisitizieni juu ya Maswahaba wangu, msiwatendee kinyume baada yangu, na yoyote atakayewapenda basi atakuwa

amewapenda kwa kunipenda meme, na mwenyekuwachukia, basi kwa kunichukia mimi atakuwa amewachukia wao pia. Na takayewaudhi atakuwa ameniudhi mimi na amemuudhi Mwenyezi Mungu Mtukufu, na mwenye kumuudhi Mwenyezi Mungu Mtukufu basi Mwenyezi Mungu huwa karibu ya kumchukua. Imepokelewa na Ahmad na Tirmidhiy. Na anasema Mtume S.A.W: Msiwatukane Maswahaba wangu, na kama mmoja wenu angelitoa dhahabu yenye ukubwa wa mfano wa Mlima wa Uhudi asingeweza kumfikia kiasi kidogo cha ratili moja na nusu ya mmoja wao kwa thawabu au hata nusu yake. Imepokelewa na Bukhari. Na anasema Mtume S.A.W: Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu amenichagua mimi na anakanichagulia Maswahaba wangu, na akawajaalia maswahaba kwangu kama mawaziri na wenye kuninusuru na wakwe, na yoyote atakayewatukana basi juu yake iwe laana ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Malaika wake na watu wote, hakubaliwi siku ya Kiama jema lolote. Imepokelewa katika kitabu cha Mustadraku alaa Swahiihaini.
Mtu yoyote mwenye kuiangalia Sira ya Maswahaba wa Mtume S.A.W, atatambua kwamba wao hawakufanikiwa kulifikia daraja hili la juu, na nafasi hii ya juu isipokuwa kwa nia yao njema kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu , na upendo wao wa kweli kwa Mtume S.A.W, na kupigana kwao jihadi kwa nafsi zao, na kuinusuru haki na kuilinda, na kuyatanguliza kwao masilahi ya umma mbele ya masilahi yao binafsi, na kuwa kwao na tabia njema na uzuri wa kutangamana kwao na watu wote, wakastahiki kusifiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, na wakawa na sifa aya kupendwa na Mtume S.A.W, na wakawa katika nafasi ya imani yake kwao.

Anasema Mshairi:
Wao ni wateule basi ujue uzito wao
Na kwa upeo wao ewe mwelewa ongozeka.

Kizazi cha Maswahaba kilikuwa ni mundu wa mageuzi katika uso wa maisha haya, na kuondosha dhuluma batilifu na mabavu vilivyojaa kila pembe ya Dunia hii kabla ya kuletwa Mtume Muhammad S.A.W, na wakaibadilisha Dunia kwa nuru ya Wahyi wa Mwenyezi Mungu na kuielekeza kwenye Haki, Uadilifu na Usawa kwa wote' na kwa hivyo kuwapenda Maswahaba kumekuwa ni Sunna ya Mtume S.A.W na kuwaombea Dua ni kujisogeza kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kuwafuata wao ni njia ya kutufikisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kuyachukua waliyotuachia ni fadhila.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu baada ya kuutaja wasifu wa Muhaajiriina na Answar:

**{وَالَّذِينَ جَاءُوا مِنْ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا لِلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ}**

**{Na waliokuja baada yao wanasema: Ewe Mola wetu M;ezi, Tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia kwa Imani, wala usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walioamini. Ewe Mola wetu Mlezi Hakika Wewe ni Mpole mweye kuhurumia}.**

Amesema Imamu Razi Mwenyezi Mungu amrehemu: Hakika uzito wa atakaekuja baada ya Muhajiriina na Answaari ni kuwakumbuka kwa kuwaombea Dua Maswahaba wa Mtume S.A.W na kuwaombea rehma zake Mwenyezi Mungu.

Na kwamba ni juu yetu sisi kutambua kuwa Hadithi inaizungumzia nafasi ya Maswahaba wa Mtume S.A.W na kuzielezea fadhila zao na kuuimarisha mchango wao kama ruwaza njema kwetu ambayo hatuwezi kuikwepa kwa ajili yetu, watoto wetu na vijana wetu, na kwamba hakika malezo yanayofanyika kwa kigezo chema yana athari kubwa na huweka misingi ya mfumo Maadili mema na Tabia za hali ya juu pamoja na mwenendo mzuri wenye fikra za ukati na uadilifu zitokanazo na uelewa mzuri wa Maswahaba wa Mtume S.A.W wa Dini sahihi ya Uislamu, na awe na Utu wa kipekee, mpaka awe na sifa ya kuubeba Ujumbe wa Mwenyezi Mungu na kuifikisha amana aliyonayo, na kuliongoza jahazi na uokkovu, kwa ajili ya kuuokoa Umma wa Mtume S.A.W kutokana na mkwamo wake na kuufikisha katika njia iliyonyooka na Usalama na Furaha pamoja na Utulivu na Maendeleo kwa wote.

Ninatamani kama tungeliutambua uzito wa Maswahaba wa Mtume S.A.W na nafasi yao na tukawafuata maadili yao na kuzifuata nyayo zao na tukajipatia nguvu kutoka katika historia yao na moyo wa kujitolea waliokuwa nao, na Utoaji na kijitoa nafsi zao, mali zao na Mtoto, na tukapita njia waliyoipitia wao kwa ajili ya kuujenga ulimwengu huu, na kujenga Ustaarabu na kuinufaisha nchi na watu wake kwa yale yanayoudhihirisha Uislamu wa kweli na Usamehevu wake.

Ewe Mola wetu Mlezi tunakuomba utusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia kwa Imani, na wala usitujaalie ndani ya nafsi zetu undani kwa wale walioamini, ewe Mola wetu Mlezi hakika wewe ni Mpole mwenye kuhurumia.

hakika Wewe ni Msikivu na ni Mjuzi, na utukubalie toba zetu kwani hakika Wewe ni mwingi wa Kukubali toba na ni mwingi wa Kurehemu.